**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**RIPOTI YA TATHMINI YA UTENDAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/16**

# TOLEO LA WANANCHI

Septemba, 2016

# YALIYOMO


**UJUMBE WA MWENYEKITI WA BODI YA WAKURUGENZI ........ 4**

**UJUMBE WA MTENDAJI MKUU ........ 5**

**SURA YA KWANZA ........ 6**

**1.0 UTANGULIZI ........ 6**

**1.1 Malengo na majukumu ya PPRA ........ 6**

**1.2 Dhima na Dira ya PPRA ........ 7**

**1.3 Utekelezaji wa mpango mkakati ........ 7**

**SURA YA PILI ........ 8**

**2.0 Mafanikio ........ 8**

**2.1 Kupunguza maambukizi mapya ya virusi vya Ukimwi na kuboresha huduma ........ 8**

**2.2 Kuzuia rushwa ndani ya PPRA ........ 8**

**2.3.1 Kuboresha utendaji kwenye manunuzi ya umma ........ 8**

*2.3.2 Uchunguzi wa ukiukwaji wa sheria na taratibu za manunuzi ........ 8*

*2.3.3 Uwasilishaji wa taarifa za manunuzi ........ 8*

**2.3.5 Kufungia makampuni/mtu kushiriki kwenye zabuni za umma ........ 10**

**2.3.6 Mkakati wa kujenga uwezo ........ 10**

**2.3.7 Huduma za ushauri ........ 11**

**2.3.8 Huduma ya Maktaba ........ 13**

**2.3.9 Mfumo wa uwasilishaji na upokeaji taarifa kwa njia ya kielektroniki ........ 13**

**2.3.10 Tovuti ya PPRA ........ 13**

**2.3.11 Jukwaa la majadiliano mtandaoni ........ 13**

**2.3.12 Huduma ya ujumbe mfupi wa simu ........ 13**

**2.3.13 Mfumo wa manunuzi kwa njia ya mtandao ........ 14**

**2.4 Kuimarisha uwezo wa PPRA katika kufikisha huduma kwa wadau ........ 14**

**2.4.1 Utoaji wa taarifa za manunuzi ya umma ........ 14**

**2.5 Kuboresha mazingira ya kazi na maslahi ya watumishi wa PPRA ........ 15**

**SURA YA TATU ........ 16**

**3.0 UKAGUZI WA MANUNUZI YA UMMA ........ 16**

*3.2.2 Mgawanyiko wa jumla ya thamani ya mikataba ........ 17*


*3.2.3 Thamani ya mikataba kulingana na makundi ya taasisi ........ 18*

*3.3.1 Malengo ya ukaguzi ........ 18*

**3.3.2 Uchaguzi wa taasisi na maeneo ya ukaguzi ........ 19**

**3.3.3 Aina za ukaguzi uliofanywa ... 19**
**3.4 Tenda zilizofanyiwa ukaguzi na thamani yake ... 20**
*3.4.1 Matokeo ya ukaguzi wa uzingatiaji wa sheria* ... **20**
**3.6 Ukaguzi wa viashiria vya rushwa ... 26**
*3.6.1 Matokeo ya ukaguzi wa viashiria vya rushwa kwa taasisi 64 zilizokaguliwa* ... **26**
*3.6.2 Matokeo ya tathmini ya viashiria vya rushwa kwa miradi* ... **27**
*3.6.3 Malipo yenye utata* ... **27**
*3.6.4 Makusanyo ya ushuru wa halmashauri* ... **27**
**3.7 Uhakiki wa malipo yenye utata kwa mwaka wa fedha 2014/15 ... 28**
**SURA YA NNE ... 29**
**4.0 CHANGAMOTO NA MATARAJIO ... 29**
**4.1 Changamoto ... 29**
**4.1.1 Changamoto za kisekta ... 29**
**4.1.2 Changamoto za ndani ya PPRA ... 29**
**4.1.3 Mkakati wa kukabiliana na changamoto ... 30**

## UJUMBE WA MWENYEKITI WA BODI YA WAKURUGENZI




PPRA imekuwa ikiandaa ripoti ya tathmini ya utendaji kazi kwa kila mwaka kuanzia mwaka wa fedha 2006/07. Lengo la ripoti hizi ni kuwafahamisha wadau namna PPRA ilivyotekeleza majukumu yake katika mwaka husika.

Hatahivyo, PPRA imekuwa ikipokea maoni mbalimbali kutoka kwa wadau wake kuwa ripoti hizi zimeandaliwa kwa kutumia lugha ya kitaalam ambayo ni ngumu kueleweka kwa wananchi wa kawaida.

Ni kwa mantiki hiyo na katika kutekeleza dhana ya utawala bora, kwa mara ya kwanza, PPRA imeandaa chapisho hili maalum ili kuongeza ushirikishwaji na uwezeshaji kwa wananchi, mashirika ya kijamii na wadau wengine kupata mrejesho kuhusiana na utendaji kazi wa taasisi ikiwemo matokeo ya ukaguzi uliofanywa kwenye miradi au manunuzi ya vifaa na huduma na pia kujenga uwezo wa jamii katika kufuatilia uwajibikaji wa taasisi za umma katika kutekeleza miradi mbalimbali inayotumia fedha za umma.

Kama inavyofahamika, sehemu kubwa ya bajeti ya kila mwaka ya Serikali hutumika kwenye manunuzi ya umma. Hivyo, uelewa na ushiriki wa wadau wote wakiwemo wananchi wa kawaida katika eneo hili ni jambo muhimu ili kuzuia upotevu wa fedha za umma unaoweza kutokea kutokana na manunuzi yasiyozingatia misingi mikuu ya manunuzi ya umma ambayo ni uwazi, ushindani na haki ili kupata thamani bora ya fedha kwenye manunuzi pamoja na kuendeleza wazabuni wa ndani.

Ni matumaini yangu kuwa taasisi za umma, mashirika ya kijamii, wananchi na wadau wa manunuzi watakitumia kitabu hiki kuongeza uelewa wa masuala ya manunuzi ya umma. Aidha, natarajia kitabu hiki kitasaidia kuongeza uwazi na uwajibikaji wa taasisi za umma na kuongeza hamasa kwa wadau kwenye ufuatiliaji wa miradi inayotekelezwa kwenye maeneo yao na hivyo kushiriki katika jitihada za kuleta thamani bora ya fedha katika miradi inayotekelezwa kwa fedha za umma.



Balozi Dkt. Matern Y. C. Lumbanga
**MWENYEKITI WA BODI**

## UJUMBE WA MTENDAJI MKUU



Chapisho hili linahusu tathmini ya utendaji kazi wa PPRA kwa mwaka wa fedha 2015/16. Pamoja na mambo mengine, chapisho linajumuisha matokeo ya ukaguzi uchunguzi juu ya utendaji wa taasisi za umma katika manunuzi, utekelezaji wa majukumu ya utoaji wa huduma za ushauri, na mikakati ya kuwajengea uwezo wadau mbalimbali kwenye masuala ya manunuzi ya umma.

Napenda kutumia fursa hii kulishukuru Shirika la Misaada la Marekani (USAID) kwa msaada wake wa kifedha iliofanikisha maandalizi na uchapishaji wa kijitabu hiki. Napenda pia kuishukuru bodi ya uhariri ya jarida la manunuzi ya umma, *'Tanzania Procurement Journal'*, kwa kuhariri kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kufanikisha kazi hii.

Mwisho, napenda kutambua mchango wa menejimenti na watumishi wote wa PPRA uliofanikisha kazi hii.



Dkt. Laurent M. Shirima
AFISA MTENDAJI MKUU

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Ili Serikali iweze kutimiza mahitaji ya wananchi wake, ni lazima ifanye manunuzi mbalimbali yakiwemo ya vifaa, kazi za ujenzi au huduma kwa kutumia fedha zilizotengwa kwenye bajeti yake. Kwa mujibu wa sheria ya manunuzi ya umma, taasisi nunuzi hutakiwa kuandaa mpango wa mwaka wa manunuzi sambamba na maandalizi ya bajeti ili mpango huo uendane na bajeti. Aidha, sheria ya manunuzi imeweka misingi ya manunuzi ya umma ambayo inapaswa kuzingatiwa na taasisi nunuzi. Misingi hiyo ni kuzingatia uwazi, ushindani na haki ili Serikali iweze kupata thamani bora ya fedha za umma zinazotumika.

Hivyo, dhana ya ukaguzi wa manunuzi ya umma inalenga kuhakikisha kwamba sheria na taratibu pamoja na misingi mikuu ya manunuzi hayo inazingatiwa, ili thamani bora ya fedha za umma iweze kupatikana katika miradi na huduma mbalimbali kama vile ubora wa barabara zilizojengwa, ubora na upatikanaji kwa wakati wa dawa na vifaa tiba, madarasa na vifaa vya shule, n.k.

Kijitabu hiki, pamoja na mambo mengine, kinajumuisha mambo makubwa mawili ambayo ni taarifa za jumla zinazohusiana na wajibu wa taasisi nunuzi kuwasilisha taarifa zao za manunuzi kwa PPRA, na pia matokeo ya ukaguzi wa manunuzi uliofanywa na PPRA kwa mwaka wa fedha 2015/16.

Sura ya kwanza inatoa muhtasari wa malengo na majukumu ya PPRA sambamba na taarifa kuhusiana na manunuzi yaliyofanywa na taasisi za umma kwa mwaka wa fedha 2015/16. Sehemu hii inazungumzia pia kuanza kwa utekelezaji wa mpango mkakati wa awamu ya pili na malengo yake.

Sura ya pili inahusu mafanikio katika utekelezaji wa malengo ya PPRA na Sura ya tatu inahusu matokeo ya ukaguzi kuhusiana na utendaji wa taasisi za umma katika manunuzi kwa mwaka wa fedha 2015/16.

Sura ya mwisho inahusu majumuisho ya changamoto ambazo PPRA imekabiliana nazo katika utekelezaji wa majukumu yake; pamoja na mikakati iliyojiwekea ili kuzipatia ufumbuzi na kuongeza ufanisi katika utendaji kazi.

### 1.1 Malengo na majukumu ya PPRA

PPRA imeundwa chini ya sheria ya manunuzi ya umma na imepewa uwezo na jukumu la kusimamia na kudhibiti manunuzi ya umma nchini. Miongoni mwa majukumu ya PPRA ni kufuatilia uzingatiaji na ukidhi wa sheria ya manunuzi na kufanya uchunguzi kuhusu ukiukwaji wa sheria ya manunuzi ya umma.

## 1.2 Dhima na Dira ya PPRA

**Dhima**
Kusimamia na kudhibiti mfumo wa manunuzi ya umma ili kuleta thamani bora ya fedha kwa maendeleo ya Taifa.

**Dira**
Kuwa na mfumo wa manunuzi ya umma unaozingatia uadilifu na unaohakikisha thamani bora ya fedha kwenye manunuzi.

## 1.3 Utekelezaji wa mpango mkakati

PPRA ilianza utekelezaji wa majukumu yake kwa kutumia mpango mkakati wa awamu ya pili Julai Mosi, 2015; ukiwa na malengo yafuatayo:

i) Kupunguza maambukizi mapya ya virusi vya Ukimwi na kuboresha huduma;
ii) Kuzuia rushwa ndani ya PPRA;
iii) Kuboresha utendaji kwenye manunuzi ya umma;
iv) Kuimarisha uwezo wa PPRA katika kufikisha huduma kwa wadau; na
v) Kuboresha mazingira ya kazi na maslahi ya watumishi wa PPRA.

## SURA YA PILI

## 2.0 Mafanikio

Katika mwaka husika, PPRA imepata mafanikio yafuatayo kwa kuzingatia malengo yaliyoainishwa katika mpango mkakati wake:

### 2.1 Kupunguza maambukizi mapya ya virusi vya Ukimwi na kuboresha huduma

Jumla ya watumishi 44 kati ya 81 walipatiwa elimu kuhusu maambukizi ya virusi vya Ukimwi, namna ya kujikinga na kukabiliana nao. Aidha, watumishi 38 kati ya 44 walipata huduma ya ushauri nasaha na upimaji wa hiari.

### 2.2 Kuzuia rushwa ndani ya PPRA

PPRA iliunda kamati ya maadili ambayo inaendelea kufanya kazi na mamlaka zinazohusika na masuala ya uadilifu ili kukabili masuala ya rushwa ndani ya PPRA.

#### 2.3.1 Kuboresha utendaji kwenye manunuzi ya umma

Katika eneo hili PPRA hufanya ukaguzi wa manunuzi kwa taasisi za umma, kama inavyooneshwa kwenye Sura ya tatu. Pamoja na kufanya ukaguzi wa kawaida wa utendaji wa taasisi za umma kwenye manunuzi, PPRA pia ilifanya uchunguzi kwenye taasisi kadhaa.

#### 2.3.2 Uchunguzi wa ukiukwaji wa sheria na taratibu za manunuzi

Katika mwaka wa fedha 2015/16, PPRA ilifanya uchunguzi wa tuhuma 14 zinazohusu mikataba 49 ya manunuzi inayokadiriwa kuwa na thamani ya shilingi trilioni 1.6. Uchunguzi huu uliohusisha taasisi 11 ulitokana na taarifa zilizopokewa kutoka vyanzo mbalimbali vikiwemo vyombo vya habari, taasisi za umma na wananchi wa kawaida.

Kwa ujumla Serikali imeweza kuokoa shilingi bilioni 852.62 kutokana na uchunguzi huo baada PPRA kuingilia kati na kusimamisha mchakato wa tenda mbili baada ya kuona kuwa Serikali isingepata thamani bora ya fedha kwenye manunuzi hayo.

Pia, uchunguzi huo umebaini kuwa Serikali ingeweza kuokoa takriban shilingi bilioni 62.45 kama taasisi zilizochunguzwa zingetekeleza mapendekezo yaliyotolewa na PPRA.

#### 2.3.3 Uwasilishaji wa taarifa za manunuzi

Mfumo wa ukaguzi na ufuatiliaji wa shughuli za manunuzi uliandaliwa na PPRA kwa lengo la kuwezesha ufuatiliaji wa michakato ya manununi katika taasisi za umma. Chini ya mfumo huo, taasisi za umma zinapaswa kuwasilisha PPRA mipango ya manunuzi ya mwaka na ripoti za maendeleo ya utekelezaji wa manunuzi. Katika mwaka wa fedha 2015/16 jumla ya taasisi 441, sawa na asilimia 98.7 ya taasisi zote,

ziliwasilisha mpango huo PPRA. Taasisi 237 ziliwasilisha PPRA tangazo la jumla la manunuzi ya mwaka husika kwa ajili ya kuchapishwa kwenye jarida la manunuzi na tovuti ambapo jumla matangazo ya tenda 1,280. Pia, PPRA ilichapokea na kuchapisha taarifa 1,977 za mikataba ya manunuzi kutoka taasisi za umma 161. Uchambuzi wa taarifa hizo umeainishwa katika **Jedwali namba 2-1:**


**Jedwali 2-1: Taarifa za mikataba**

| Na. | Makundi ya taasisi | Idadi ya taasisi zilizowasilisha | Idadi ya taarifa zilizopokewa | Thamani ya mikataba (Shilingi bilioni) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Halmashauri | 36 | 316 | 76.49 |
| 2 | Wizara | 14 | 229 | 102.76 |
| 3 | Mashirika ya Umma | 54 | 661 | 474.21 |
| 4 | Wakala/Mamlaka | 42 | 627 | 250.65 |
| 5 | Idara zinazojitegemea | 13 | 141 | 123.23 |
| 6 | Ofisi za wakuu wa mikoa | 2 | 3 | 0. 54 |
| | **Jumla** | **161** | **1,977** | **1,027.88** |

Uchambuzi wa taarifa za mikataba kulingana na aina ya manunuzi unaoneshwa kwenye **Jedwali 2-2:**

**Jedwali 2-2: Taarifa za mikataba na aina ya manunuzi**

| Na. | Aina ya manunuzi | Idadi ya taarifa za mikataba | Thamani ya mikataba (Shilingi bilioni) |
|---|---|---|---|
| 1 | Kazi za ujenzi | 742 | 645.61 |
| 2 | Bidhaa | 572 | 248.21 |
| 3 | Huduma za ushauri wa kitaalam | 131 | 44.84 |
| 4 | Huduma zisizohitaji ushauri wa kitaalam | 532 | 89.22 |
| | **Jumla** | **1,977** | 1,027.88 |



### 2.3.4 Tathmini ya uwezo wa kufanya manunuzi

PPRA inatoa fursa kwa taasisi kufanyiwa tathmini ya uwezo wake wa kufanya manunuzi. Chini ya utaratibu huu, kwa hiari yake, taasisi hufanyiwa tathmini na kupewa ushauri wa namna ya kuboresha mfumo na taratibu zake za manunuzi ili kupata thamani bora ya fedha. Katika mwaka wa fedha 2015/16, Mfuko wa Bima ya Afya ni taasisi pekee iliyonufaika na huduma hiyo.

### 2.3.4 Ushirikiano na taasisi nyingine

Katika kutekeleza majukumu yake, PPRA inashirikiana na taasisi nyingine ili kuhakikisha manunuzi ya umma yanakuwa na tija kwa maendeleo ya nchi. Ushirikiano huu hutekelezwa kwa makubaliano maalum kati yake na taasisi hizo.

Katika mwaka 2015/16, PPRA iliingia makubaliano na Chuo cha Serikali za Mitaa - Hombolo, Tume ya Ushindani, Wakala wa Usajili wa Kampuni, Mamlaka ya Chakula na Dawa, Shirika la Viwango Tanzani pamoja na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali.

### 2.3.5 Kufungia makampuni/mtu kushiriki kwenye zabuni za umma

Katika mwaka wa fedha 2015/16 PPRA iliandaa mwongozo wa kuendesha taratibu za kufungia wazabuni kushiriki kwenye zabuni za umma kutokana sababu mbalimbali zikiwemo vitendo vya udanganyifu katika michakato ya manunuzi, kutotekelezwa kwa tamko la dhamana ya zabuni na kukiuka vigezo na masharti ya mikataba.

### 2.3.6 Mkakati wa kujenga uwezo

Katika mwaka wa fedha 2015/16, PPRA iliendelea kutekeleza mkakati wake wa kujenga uwezo kwa kutoa mafunzo kwa makundi mbalimbali kuhusu sheria ya manunuzi ya umma kama ifuatavyo:

#### a) Mafunzo

Mafunzo kuhusiana na sheria ya manunuzi ya umma yalitolewa kwa watumishi wa taasisi za umma, ofisi za wakuu wa mikoa, na halmashauri kama ifuatavyo:

Watumishi 629 kutoka taasisi 29 walipatiwa mafunzo maalum ya sheria ya manunuzi ikilinganishwa na watumishi 139 kutoka taasisi 11 waliopatiwa mafunzo hayo mwaka uliopita.

Pia PPRA ilitoa mafunzo kwa wataalam 98 wanaoshughulika na manunuzi ya umma na usimamizi wa fedha kutoka ofisi za wakuu wa mikoa na halmashauri zilizopoka katika mikoa ya Simiyu, Geita, Dodoma, Rukwa, Mtwara, Kigoma, Ruvuma, Katavi, Njombe na Mara. Lengo la mafunzo hayo lilikuwa kuwapatia washiriki uelewa wa sheria na usimamizi wa masuala ya manunuzi.

Aidha, washiriki 53 kutoka asasi za kiraia na vyombo vya habari walihudhuria mafunzo na majadiliano yaliyolenga kuhamasisha utekelezaji wa wajibu wao katika manunuzi ya umma.




**b) Kongamano la Manunuzi ya Umma**

Katika mwaka wa fedha 2015/16, PPRA iliandaa Kongamano la Mwaka la Manunuzi ya Umma ambapo wadau walijadili utekelezaji wa sheria ya manunuzi na kanuni zake. Kongamano hilo lilihudhuriwa na washiriki 430 wakiwemo madiwani, wajumbe wa bodi za wakurugenzi za mashirika ya umma, watendaji wakuu wa taasisi za umma pamoja na wajumbe wa bodi za zabuni. Washiriki wengine walitoka idara tumizi na vitengo vya usimamizi wa manunuzi na ukaguzi wa ndani.

**c) Kongamano la Manunuzi ya Umma Afrika Mashariki**

PPRA ilikuwa mwenyeji wa kongamano la nane la manunuzi ya umma kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki lililofanyika Arusha kuanzia tarehe 2 hadi 4 Septemba, 2015 ambapo washiriki 220 walihudhuria.

Kongamano hilo ni jukwaa linaloratibiwa na taasisi za usimamizi wa manunuzi ya umma na huvutia wadau mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi wanachama wa Jumuiya hiyo wakiwemo washiriki kutoka taasisi za umma na binafsi pamoja na asasi za kiraia na vyombo vya habari.

### 2.3.7 Huduma za ushauri

Katika mwaka wa fedha 2015/16, PPRA iliendelea kutoa huduma ya ushauri kwenye masuala mbalimbali yahusuyo manunuzi ya umma. Kwa mfano, jumla ya maombi 30 ya uhalalisho wa manunuzi ya dharura yalishughulikiwa, hatua za kinidhamu zilipendekezwa dhidi ya watumishi kutoka bodi ya zabuni, vitengo vya manunuzi na

kamati za tathmini kwa kuisababishia Serikali hasara kufuatia maamuzi yaliyotolewa na Mamlaka ya Rufani za Zabuni za Umma.

Pia, PPRA ilishiriki kikamilifu katika mchakato wa marekebisho ya sheria ya manunuzi ya umma kwa kutoa mchango wake katika marekebisho hayo. Mambo muhimu yaliyozingatiwa ni pamoja na;

i) Bei kubwa za bidhaa, kazi za kandarasi na huduma zisizolingana na bei ya soko;
ii) Gharama kubwa zinazotokana na michakato ya manunuzi;
iii) Michakato ya manunuzi kuchukua muda mrefu;
iv) Kiwango kidogo cha uwajibikaji na weledi;
v) Vikwazo kwa makampuni au taasisi za umma zinazojiendesha kibiashara;
vi) Kutokuwepo kwa msawazisho wa vifaa na huduma zinazotumika Serikalini;
vii) Tofauti kati ya taratibu za manunuzi zinazotumiwa na halmashauri na zile zinazotumiwa na taasisi nyingine za umma; na
viii) Mgongano wa maslahi na muingiliano wa majukumu katika michakato ya manunuzi.

Matokeo yanayotarajiwa ya mabadiliko ya sheria ya manunuzi ya umma ni kuongeza ufanisi kwa kupunguza gharama na muda wa uendeshaji wa michakato ya manunuzi, Serikali kununua bidhaa na huduma kwa bei inayoendana na bei ya soko, Serikali kunufaika na ununuzi wa mahitaji ya aina chache kwa mfumo wa ununuzi wa pamoja, kupungua kwa mianya ya rushwa na kuongezeka kwa uwajibikaji katika michakato ya zabuni pamoja na kuweka mfumo utakaotoa upendeleo kwa makundi maalum kushiriki katika michakato ya zabuni za umma.



### 2.3.8 Huduma ya Maktaba

Katika mwaka wa fedha 2015/16 huduma za maktaba ziliboreshwa kwa kusimika mfumo wa Tehama ambao unarahisha shughuli zote za maktaba ikiwemo kuchagua, kuagiza na kuandaa machapisho. Maktaba inahudumia watafiti, wanataaluma, wadau wa masuala ya ununuzi wa umma na wananchi kwa ujumla.

### 2.3.9 Mfumo wa uwasilishaji na upokeaji taarifa kwa njia ya kielektroniki

PPRA iliendelea kuboresha mfumo wake wa uwasilishaji na upokeaji wa taarifa kwa njia ya kielektroniki ili kukidhi mahitaji ya kisheria. Aidha, maofisa 488 kutoka taasisi 291 walipatiwa mafunzo ya utumiaji wa mfumo huo.

Kutokana na mafunzo hayo, idadi ya watumiaji wa mfumo waliosajiliwa ilifikia 1,518, kutoka 1,143 kwa mwaka uliopita.

### 2.3.10 Tovuti ya PPRA

Wadau wa manunuzi waliendelea kutumia tovuti ya PPRA **(www.ppra.go.tz)** na ubao wa matangazo ya tenda ili kupata taarifa mbalimbali za tenda. Jumla ya matangazo ya tenda 5,039 yaliwekwa kwenye tovuti.

### 2.3.11 Jukwaa la majadiliano mtandaoni

Jukwaa hili linalopatikana katika tovuti ya PPRA, lilianzishwa mwaka 2009 ili kuwezesha wadau kujadiliana na kubadilishana uzoefu kuhusu manunuzi ya umma. Kwa mwaka 2015/16, watumiaji 844 waliandikishwa ikilinganishwa na 801 wa mwaka uliopita.

### 2.3.12 Huduma ya ujumbe mfupi wa simu

PPRA iliendelea kuboresha huduma ya ujumbe mfupi wa simu za kiganjani ulioanzishwa kwa lengo la kuwawezesha wazabuni kupokea taarifa za tenda. Mzabuni anaweza kujiunga na huduma hii kwa kutuma ujumbe mfupi kupitia namba **15332.**




### 2.3.13 Mfumo wa manunuzi kwa njia ya mtandao

Kwa mwaka 2015/16, PPRA iliendelea na maandalizi ya mfumo wa manunuzi kwa njia ya mtandao ikiwa ni pamoja na kuwaelimisha wadau kuhusu mfumo huo. Aidha, mkataba wa usimikaji na utekelezaji wa mfumo ulisainiwa mwezi Mei, 2016 kati ya Serikali na mkandarasi ambapo mfumo huo utaanza kwa majaribio ya ununuzi wa dawa, vifaa tiba na bidhaa mtambuka.

## 2.4 Kuimarisha uwezo wa PPRA katika kufikisha huduma kwa wadau

### 2.4.1 Utoaji wa taarifa za manunuzi ya umma

***a) Sera ya mawasiliano***

Katika mwaka wa fedha 2015/16, PPRA iliandaa Sera ya Mawasiliano pamoja na mkakati wa utekelezaji wake. Sera hii inatumiwa kama mwongozo wa mawasiliano kati ya PPRA na wadau wake.

***b) Tuzo za umahiri wa uandishi wa habari za manunuzi***

Katika jitihada zake za kuongeza uelewa wa wadau kuhusu manunuzi, PPRA ilishirikiana na Baraza la Habari Tanzania kuanzisha tuzo ya mwandishi bora wa habari za manunuzi kupitia tuzo za umahiri wa uandishi wa habari Tanzania. PPRA ilidhamini tuzo hiyo kwa msaada wa serikali ya Ubelgiji kupitia shirika lake la maendeleo ya kiufundi (BTC).

*c) Tanzania Procurement Journal*

Jarida la *Tanzania Procurement Journal* hutumiwa na wadau wa manunuzi kama kituo cha taarifa zote za manunuzi ya umma. Katika mwaka wa fedha 2015/16, PPRA iliandaa matoleo 52 na kuchapisha nakala 780,000 zikiwa na taarifa za matangazo mbalimbali ya tenda pamoja na ripoti za ukaguzi wa manunuzi. Nakala hizi zilisambazwa nchi nzima kila siku ya Jumanne kupitia gazeti la *Daily News*.




*d) Vipindi vya elimu kwa umma*

Ili kutoa elimu kwa umma, PPRA iliandaa matangazo ya redio na televisheni juu ya uadilifu na madhara ya rushwa kwenye manunuzi ya umma. Matangazo hayo yanatarajiwa kurushwa katika vituo mbalimbali vya redio na televisheni hapa nchini baadaye mwaka huu. Aidha, PPRA iliandaa na kuchapisha toleo la wananchi la ripoti ya ukaguzi wa manunuzi ya umma kwa mwaka wa fedha 2014/15.

**2.5 Kuboresha mazingira ya kazi na maslahi ya watumishi wa PPRA**

Mamlaka iliendelea kuboresha mazingira bora ya kazi, mifumo, vitendea kazi kwa ajili ya kuongeza motisha ya wafanyakazi wake ili waweze kutoa mchango wao kuisaidia Mamlaka kufikia malengo yake.

## SURA YA TATU

## 3.0 UKAGUZI WA MANUNUZI YA UMMA

### 3.1 Idadi ya mikataba ya manunuzi

Katika mwaka wa fedha 2015/16, taasisi 322 kati ya 493 sawa na asilimia 65.31 ziliwasilisha taarifa za mikataba yao PPRA. Kiwango cha uwasilishaji wa taarifa hizo kiliongezeka ikilinganishwa na mwaka uliopita ambapo taasisi 267 kati ya 469 sawa na asilimia 57, ziliwasilisha. Uchambuzi wa idadi ya mikataba iliyowasilishwa umeainishwa kwenye **Jedwali 3.1.**

**Jedwali 3-1:** Uchambuzi wa idadi na aina ya mikataba

| Na. | Aina za mikataba | Idadi ya mikataba | Asilimia ya jumla ya tuzo za mikataba iliyotolewa |
|---|---|---|---|
| 1 | Bidhaa | 70,713 | 64.6 |
| 2. | Kazi za ujenzi | 3,970 | 3.6 |
| 3. | Huduma za ushauri wa kitaalam | 779 | 0.7 |
| 4. | Huduma zisizohitaji ushauri wa kitaalam | 34,003 | 31 |
| 5. | Uuzaji wa mali za Serikali kwa njia ya tenda | 110 | 0.1 |
| | **Jumla** | **109,575** | **100** |

### 3.2 Thamani ya mikataba ya manunuzi

Uchambuzi wa taarifa kuhusu thamani ya mikataba unaonesha taswira halisi ya manunuzi yanayofanywa na Serikali kwani taasisi 25 zilizokuwa na matumizi makubwa ni miongoni mwa taasisi zilizowasilisha taarifa hizo.

Kila moja ya taasisi hizo 25 ilifanya manunuzi yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 20 katika mwaka wa fedha 2015/16. Idadi ya mikataba iliyotolewa na taasisi hizo katika kipindi cha miaka saba iliyopita ilikuwa kati ya asilimia 70 na 85 ya thamani ya manunuzi yote ya Serikali. Uchambuzi zaidi wa taarifa za idadi ya mikataba unaoneshwa kwenye **Jedwali 3.1.**

**Jedwali 3-2: Mchanganuo wa tuzo za mikataba ya manunuzi**

| Mwaka wa fedha | Idadi ya taasisi ambazo taarifa za mikataba yake zilipokewa | Idadi ya taarifa za mikataba zilizopokewa | Thamani ya mikataba iliyopokewa (TZS Bilioni) | Jumla ya bajeti (TZS Bilioni) |
|---|---|---|---|---|
| 2013/14 | 235 | 74,208 | 4,859 | 18,249 |
| 2014/15 | 267 | 75,509 | 4,349 | 19,853 |
| 2015/16 | 322 | 109,575 | 3,001 | 22,495.5 |

Kiwango kikubwa cha mikataba kilikuwa kwa njia ya manunuzi madogomadogo (yaani yasiyozidi shilingi milioni 10) na mikataba ya manunuzi ya bidhaa na huduma mtambuka.

Mikataba 59,492 yenye thamani ya shilingi bilioni 213.90 iliingiwa kwa njia ya manunuzi madogomadogo; mikataba 30,296 yenye thamani ya shilingi bilioni 203.80 ilitumia njia ya mikataba ya manunuzi ya bidhaa na huduma mtambuka; na mikataba 19,762 yenye thamani ya shilingi bilioni 2,582.80 iliingiwa kwa njia ya ushindani.




### 3.2.1 Uwiano wa bajeti na manunuzi yaliyofanywa

Uchambuzi wa taarifa za bajeti zilizowasilishwa na taasisi hizo 250 unaonesha kuwa kiasi cha shilingi trilioni 7.31 kilipokewa au kukusanywa ambayo ni sawa na asilimia 60 ya bajeti ya shilingi trilioni 12.13 iliyoidhinishwa. Aidha, uchambuzi zaidi unaonesha kuwa shilingi trilioni 2.70 kati ya fedha iliyopokewa au kukusanywa zilitumika kwenye manunuzi.

Katika mwaka husika, uwiano wa kiwango cha fedha kilichotumika kwenye manunuzi dhidi ya mapato yaliyokusanywa kilishuka kwa asilimia 3 ikilinganishwa na mwaka uliopita ambapo taasisi za umma 267 kati ya 469 ziliwasilisha taarifa zao.

### 3.2.2 Mgawanyiko wa jumla ya thamani ya mikataba

Mgawanyiko wa thamani ya mikataba kwa taasisi 322 unaonesha kwamba katika shilingi trilioni 2.70 zilizotumika kwenye manunuzi, asilimia 44.6 ilitumika kwenye miradi ya kazi za ujenzi, asilimia 38.9 kwenye manunuzi ya vifaa, asilimia 7.6 kwenye huduma za ushauri wa kitaalam, asilimia 8.9 huduma zisizohitaji ushauri wa kitaalam na asilimia 0.01 kwenye uuzaji wa mali za umma kwa njia ya tenda.

Jumla ya thamani ya manunuzi yaliyofanywa na Tanesco, Tanroads na PPF ilikuwa shilingi trilioni 1.09. Sehemu kubwa ya manunuzi ilikuwa ya kazi za ujenzi zilizofanywa na Tanroads na PPF ikifuatiwa na manunuzi ya bidhaa yaliyofanywa na Tanesco.

### 3.2.3 Thamani ya mikataba kulingana na makundi ya taasisi

Mchanganuo wa jumla ya fedha iliyotumika kwenye manunuzi katika asilimia ni kama ifuatavyo:

i) Mashirika ya umma, asilimia 43.5;
ii) Wakala wa serikali na mamlaka za maji, asilimia 28;
iii) Wizara, asilimia 12.8;
iv) Halmashauri, asilimia 10.7;
v) Idara zinazojitegemea, asilimia 4.5; na
vi) Ofisi za wakuu wa mikoa, asilimia 0.5.

## 3.3 Matokeo ya ukaguzi wa manunuzi

### 3.3.1 Malengo ya ukaguzi

Sheria ya manunuzi ya umma imeipa PPRA mamlaka ya kufanya ukaguzi wa manunuzi yanayofanywa na taasisi za umma kuanzia wakati wa mchakato wa tenda, utekelezaji wa mikataba na baada ya kukamilika kwa mikataba.

Malengo ya ukaguzi, pamoja na mambo mengine, ni kuangalia iwapo taratibu, mifumo na michakato ya manunuzi ilizingatia na kufuata sheria ya manunuzi ya umma, na iwapo miradi iliyotekelezwa ilileta matokeo yaliyokusudiwa kulingana na thamani ya fedha iliyotumika.

PPRA ilifanya ukaguzi wa manunuzi na uhakiki kwa taasisi 70; zikiwemo taasisi 15 zilizopo kwenye kundi la wizara, idara zinazojitegemea na wakala wa serikali; halmashauri 25 na mashirika ya umma 30.

Taasisi 26 zilifanyiwa ukaguzi wa uzingatiaji wa sheria tu, taasisi 36 zilifanyiwa ukaguzi wa uzingatiaji wa sheria pamoja na kupima thamani ya fedha kwenye miradi. Aidha, taasisi sita zilifanyiwa ukaguzi wa uzingatiaji wa sheria pamoja na kupima utekelezaji wa mapendekezo ya PPRA ya mwaka uliotangulia.

Ukaguzi huu ulihusu manunuzi yaliyofanywa na taasisi za umma katika mwaka wa fedha 2015/16, na pia kupima utekelezaji wa mapendekezo ya PPRA ya mwaka wa fedha 2014/15.




### 3.3.2 Uchaguzi wa taasisi na maeneo ya ukaguzi

Uchaguzi wa taasisi kwa ajili ya kufanyiwa ukaguzi ulizingatia uwepo wa vihatarishi. Taasisi ambazo jumla ya thamani ya manunuzi yake ilizidi shilingi bilioni 20 zilijumuishwa moja kwa moja kwenye ukaguzi; wakati taasisi nyingine zilichaguliwa kwa kuzingatia kigezo kimoja au zaidi kati ya vifuatavyo:

i) Taasisi ambazo ziliripotiwa mara kwa mara kuhusiana na ukiukwaji wa taratibu za manunuzi; pamoja na taasisi zilizokuwa na tuhuma zilizosababisha kufanyiwa uchunguzi na PPRA;
ii) Taasisi zilizopata maksi za chini katika ukaguzi uliopita;
iii) Taasisi ambazo hazikuwa zimekaguliwa kwa muda mrefu; na
iv) Kwa taasisi yoyote iliyo jirani na taasisi inayofanyiwa ukaguzi.

### 3.3.3 Aina za ukaguzi uliofanywa

*a) Ukaguzi wa uzingatiaji wa sheria*

Ukaguzi huu ulilenga aina za manunuzi na njia zilizotumika kufanya manunuzi hayo pamoja na thamani ya mikataba iliyoingiwa. Aidha, ukaguzi uliangalia manunuzi yenye gharama kubwa na yenye athari ya upotevu wa fedha za umma kama vile manunuzi toka kwa mzabuni mmoja, manunuzi ya dharura, manunuzi yasiyokuwa na kibali, manunuzi yasiyokuwa kwenye mpango wa manunuzi wa taasisi na yale yaliyofanywa kwa njia zisizo sahihi.

*b) Ukaguzi wa kupima thamani ya fedha kwenye miradi*

Ukaguzi huu ulilenga miradi iliyotekelezwa kwa kuangalia utekelezaji wa mikataba ya bidhaa, kazi za ujenzi na huduma za ushauri wa kitaalam. Aidha, ukaguzi uliangalia njia zilizotumika kuendesha tenda, iwapo mkataba wa tenda ulisainiwa katika mwaka wa fedha 2015/16, thamani ya mikataba midogo na mikubwa iliyoingiwa na iwapo mradi ulikuwa wa barabara, madaraja, majengo, miradi ya maji, pamoja na vifaa vya kompyuta.

*c) Udanganyifu na rushwa kwenye manunuzi ya umma*

Masuala ya udanganyifu na rushwa katika manunuzi ya umma yalifuatiliwa kwa kuzingatia makubaliano kati ya PPRA na Takukuru. Katika makubaliano hayo, viashiria kadhaa vya rushwa vimeainishwa ambavyo PPRA huvitumia katika ukaguzi wake. Viashiria hivyo vikiwa vingi ni ishara ya uwepo wa vitendo vya rushwa na udanganyifu kwenye tenda husika.

Ni muhimu kutambua kwamba ugunduzi wa viashiria vya rushwa kwenye manunuzi siyo ushahidi pekee wa rushwa kwenye manunuzi husika. Viashiria vya rushwa katika taasisi au mradi vinapokuwa vingi, PPRA hupeleka Takukuru ripoti ya ukaguzi ya taasisi husika kwa uchunguzi zaidi.

### 3.4 Tenda zilizofanyiwa ukaguzi na thamani yake

**Jedwali 3-3** linaonesha aina ya tenda, idadi, thamani pamoja na mchanganuo kwa asilimia.

**Jedwali 3-3: Tenda ziliyofanyiwa ukaguzi**

| Na | Tenda | Idadi ya tenda | Thamani ya tenda (shilingi bilioni) | Thamani ya tenda kwa asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ujenzi | 740 | 345.02 | 17.0 |
| 2 | Vifaa | 7,136 | 1,513.49 | 74.8 |
| 3 | Kazi za ushauri wa kitaalamu | 85 | 76.61 | 3.8 |
| 4 | Kazi zisizohitaji ushauri wa kitaalamu | 9,625 | 46.33 | 2.3 |
| 5 | Manunuzi madogomadogo | 1,757 | 40.39 | 2.0 |
| 6 | Kazi za ujenzi zinazotumia wataalam waliomo ndani ya taasisi | 148 | 1.53 | 0.1 |
| | **Jumla** | **19,491** | **2,023.37** | **100** |

#### *3.4.1 Matokeo ya ukaguzi wa uzingatiaji wa sheria*

Wastani wa jumla wa uzingatiaji wa sheria ya manunuzi kwa taasisi zilizokaguliwa ni maksi 71, kiwango ambao ni wa juu ikilinganishwa na wastani wa mwaka uliopita, ambao ulikuwa maksi 69. Hata hivyo, wastani huo wa maksi 71 uko chini ya lengo lililowekwa, yaani maksi 78.

Uchambuzi unaonesha kwamba taasisi za umma 10 kati ya 70 zilipata kiwango kisichoridhisha katika uzingatiaji wa sheria, yaani chini ya maksi 60. Taasisi 38 zilipata kiwango cha kati, yaani maksi 60 hadi 77 ambapo taasisi 22 zilipata kiwango cha kuridhisha, yaani maksi 78 na zaidi. Taasisi zilizopata alama zisizoridhisha ni pamoja na Taasisi ya Uzalishaji (NIP), Dar es Salaam Rapid Transist (DART), Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Makumbusho ya Taifa, Halmashauri ya jiji la Dar es Salaam, Halmashauri ya jiji la Mwanza, Kampuni ya Reli Tanzania (TRL), Taasisi ya Mifupa (MOI), Halmashauri ya Manispaa ya Musoma na Mamlaka ya Maji safi na Maji taka - Bukoba (BUWASA).

Vigezo vilivyotumika kupima uzingatiaji wa sheria vilikuwa saba ambavyo ni:

i) Muundo wa uendeshaji manunuzi kitaasisi;
ii) Uandaaji na utekelezaji wa mpango wa manunuzi;
iii) Uendeshaji wa michakato ya tenda;
iv) Usimamizi wa mikataba;
v) Utunzaji wa nyaraka za tenda;
vi) Utumiaji wa mifumo ya PPRA; na
vii) Kushindwa kushughulikia malalamiko ya wazabuni.

Wastani wa uzingatiaji wa sheria unaonesha kuwa taasisi za umma zilifanya vizuri kwenye maeneo mawili ambayo ni; muundo wa bodi za tenda ambapo zilipata maksi 94.1 na katika uundwaji wa kitengo cha manunuzi maksi 82.4.

**a) Muundo wa uendeshaji wa manunuzi kitaasisi**

Uchambuzi wa matokeo ya ukaguzi katika kigezo hiki unaonesha kuwa na wastani mzuri (juu ya asilimia 78) katika uundwaji wa bodi za tenda, kuanzishwa vitengo vya usimamizi wa manunuzi na ukaguzi wa ndani. Hatahivyo, taasisi zilipata wastani wa kuridhisha (kati ya asilimia 60 na 77) katika kuifahamisha PPRA juu ya kuundwa kwa bodi za tenda. Taasisi zimefanya vibaya kwenye kipengele cha mafunzo kwa wajumbe wa bodi za tenda na wakaguzi wa ndani.

**b) Uandaaji na utekelezaji wa mpango wa manunuzi wa mwaka**

Ukaguzi ulibaini kuwa uandaaji na utekelezaji wa mpango wa manunuzi ulikuwa wa kuridhisha, kwani taasisi zilipata maksi 82 katika uzingatiaji wa sheria.

Hata hivyo, upungufu ulibainika katika uwasilishaji wa mpango wa manunuzi kwa ajili ya kuchapishwa kwenye jarida la manunuzi la *Tanzania Procurement Journal* na katika tovuti ya PPRA, kwani taasisi zilipata maksi 66 na utekelezaji sahihi wa mpango wa manunuzi wa mwaka iliyopata maksi 72.

**c) Usahihi katika michakato ya tenda**

Ukaguzi katika sehemu hii ulibaini mambo yafuatayo:

- Taasisi 64 zilipata wastani wa maksi 76.1, kiwango kilicho chini ya lengo; na
- Taasisi zilipata wastani wa maksi 78 katika viwango vingine vidogovidogo 14 kati ya 20, ambacho ni kiwango cha kuridhisha.

**d) Usimamizi katika utekelezaji wa mikataba**

Uzingatiaji wa sheria katika kigezo hiki ulipata maksi 72 ambazo ni chini ya kiwango kilicholengwa cha asilimia 78.

Aidha, taasisi zilipata kiwango cha kuridhisha katika vigezo vya ukamilishaji wa nyaraka za zabuni, idhini ya bodi ya tenda na uwasilishwaji wa mikataba kwa Mwanasheria mkuu wa Serikali.

Yafuatayo ni matokeo katika vigezo vingine:

i) Maksi 64.1 katika uwepo wa mpango wa uhakika wa ubora;
ii) Maksi 62.2 katika uzingatiaji wa mpango wa uhakika wa ubora;
iii) Maksi 63.6 katika upatikanaji wa na ubora wa ripoti za utekelezaji wa mikataba;
iv) Maksi 66.6 katika ufanyikaji wa vikao vya menejimenti, uandaaji wa nyaraka na utiaji saini na;
v) Maksi 53.4 katika uandaaji wa ripoti ya utekelezaji wa miradi.

**e) Utunzaji wa kumbukumbu za manunuzi**

Mambo yaliyoangaliwa kwenye kigezo hiki ni kama kumbukumbu kamili zilikuwepo na pia kama zilitunzwa vizuri. Kwa ujumla, taasisi zilipata wastani wa maksi 70 ambazo ni chini ya kiwango kilicholengwa.

Udhaifu katika eneo hili ulikuwa ukosefu wa sehemu ya kutosha ya kuhifadhia kumbukumbu, hali iliyosababisha nyaraka za manunuzi kusambaa kwenye idara mbalimbali. Taasisi zilifanya vibaya, hususan katika kigezo cha mpangilio wa kumbukumbu za manunuzi.

**f) Matumizi ya mifumo ya PPRA**

Kwa wastani taasisi zilifanya vibaya katika kigezo hiki kwa kupata wastani wa asilimia 38, ikiimaanisha kuwa nyingi hazikutumia mifumo ya PPRA ya kuwasilisha taarifa za manunuzi kwa mfumo wa kielektroniki pamoja na ule wa ufuatiliaji na usimamizi wa shughuli za manunuzi.

Aidha, taasisi zilionesha kiwango cha kati katika uwasilishaji wa mpango wa manunuzi wa mwaka kwa kutumia mfumo wa PPRA kwa kupata asilimia 68, huku zikifanya vibaya katika uwasilishaji wa ripoti za tenda, uwasilishaji wa ripoti za manunuzi na za utekelezaji wa tenda.

**g) Ushughulikiaji wa malalamiko**

Taasisi pia zilikaguliwa kuona jinsi zilivyoshughulikia malalamiko ya wazabuni wakati wa michakato. Katika kigezo hiki, taasisi nunuzi ziliadhibiwa kwa kupokwa hadi maksi kumi pale ilipobainika kuwa zilishindwa kushughulikia malalamiko hayo.

Katika taasisi 70 zilizokaguliwa, taasisi tano zilipokwa maksi hizo kwa kushindwa kushughulikia malalamiko inavyopaswa.

## 3.5 Matokeo ya ukaguzi wa kupima thamani ya fedha

Vigezo vitano vilitumika katika kupima kama thamani halisi ya fedha ilipatikana kwenye miradi ya ujenzi. Vigezo hivyo ni:

i) Uandaaji, usanifu na utunzaji wa nyaraka za tenda;
ii) Mchakato wa manunuzi;
iii) Usimamiaji wakati wa utekelezaji wa miradi ya ujenzi;
iv) Ubora na ukubwa wa miradi ya ujenzi iliyotekelezwa; na
v) Ufungaji na ukamilishaji wa miradi.

**(a) Uandaaji, usanifu na utunzaji wa nyaraka za tenda**

Matokeo ya jumla yalionesha kiwango cha kuridhisha kwa kupata maksi 82.8 ambazo ni juu ya lengo la asilimia 75.

Hata hivyo, kulibainika udhaifu kama ifuatavyo:

i) Uteuzi wa msimamizi wa miradi ulifanywa baada ya mradi kuanza;
ii) Kulikuwapo makadirio yaliyozidi uhalisia wa mahitaji katika vifaa;
iii) Kukosekana kwa michoro ya miradi au michoro inayojitosheleza;
iv) Makadirio ya kihandisi yasiyo na uhalisia wa gharama;
v) Kukosekana kwa makadirio ya mhandisi, mchoro sanifu, mahitaji ya mradi, malengo ya viwango vya ubora; na
vi) Uchambuzi yakinifu kutokuzingatia programu maalum ya ukarabati wa barabara.

**(b) Usahihi katika mchakato wa tenda**

Matokeo ya jumla katika kigezo hiki yalionesha kuwa taasisi zilipata maksi 80.1 ambacho ni kiwango cha kuridhisha.

Hata hivyo, udhaifu ulibainika katika kigezo hiki kama ifuatavyo:

i) Kulikwa na uchelewaji katika kuingia mikataba;
ii) Kushindwa kuwataarifu wazabuni walioshindwa juu ya matokeo ya tenda;
iii) Notisi ya kutoa tuzo ya mkataba haikutolewa;
iv) Tenda zilitolewa nje ya muda halali;
v) Gharama halisi za uharibu zilizoainishwa kwenye mkataba hazikuzingatia sheria ya manunuzi ya umma;
vi) Kutowasilisha PPRA taarifa za tenda kwa ajili ya kuchapisha kwenye jarida la manunuzi la Tanzania Procurement Journal na tovuti ya PPRA;
vii) Mabadiliko ya mikataba hayakuidhinishwa na bodi ya tenda;
viii) Ripoti za tathmini za tenda zilikuwa na upungufu
ix) Kukosekana kwa uthibitisho kwamba mikataba kusainiwa na mwanasheria mkuu wa Serikali.

**(c) Usimamizi wa kazi za ujenzi na utekelezaji wa mikataba**


Katika miradi ya ujenzi, uchambuzi ulipima kiwango cha usimamizi na utimilifu wa masharti ya mikataba.

Matokeo ya jumla yalionesha kuwa taasisi zilipata wastani wa maksi 67.3 ambacho ni kiwango cha kuridhisha. Hata hivyo, upungufu uliobainika usipoondolewa taasisi husika hazitafanikisha lengo la upatikanaji wa thamani halisi ya fedha.

Miradi 23 au asilimia 14.7 ya miradi iliyokaguliwa, ilikuwa na kiwango katika upatikanaji wa thamani ya fedha.

Baadhi ya miradi ilikuwa na upungufu ufuatao:

i) Wakandarasi na watoa huduma za ushauri wa kitaalam hawakuweka bima dhidi ya miradi husika, kinyume na matakwa ya mikataba;
ii) Bondi na bima za miradi ambazo ziliainishwa kwenye mikataba, hazikuwasilishwa kwa taasisi;
iii) Taasisi hazikuteua wasimamizi wa miradi;
iv) Ucheleweshwaji wa malipo ya makandarasi na watoa huduma;
v) Kuchelewa kuanza kwa kazi baada ya kukabidhiwa eneo la mradi;
vi) Kutoandaliwa kwa mpango wa uhakiki wa ubora wa miradi;
vii) Ukosefu wa ushahidi wa kufanyika kwa mikutano eneo la mradi;
viii) Kutokuwepo ratiba ya kazi ya mkandarasi;
ix) Usimamizi mbovu wa miradi; na
x) Kufanyika malipo yenye utata.




**(d) Utimilifu na ukamilishaji wa miradi**

Tathmini ilifanywa kwenye miradi iliyokamilika ili kubaini ubora na utimilifu wa majengo kwa mujibu wa michoro, orodha ya maeneo yaliyokuwa na utata, utoaji wa hati ya utimilifu wa miradi, hati ya mwisho, kipindi cha matazamio, uandaaji wa taarifa ya mwisho ya kufunga mradi pamoja na malipo ya mwisho.

Matokeo ya ujumla katika kigezo hiki yalionesha kiwango cha kuridhirisha, cha wastani wa maksi 81. Hata hivyo, miradi tisa kati ya 157 iliyokaguliwa, sawa na asilimia 5.7, ilifanya vibaya katika kigezo hiki.
Upungufu ulibainika kama ifuatavyo:

i) Usimamizi mbaya wa miradi;
ii) Kutokuwepo kwa mpango wa kuhakiki ubora;
iii) Kutokuwepo kwa vielelezo vya kufanyika vikao eneo la mradi;
iv) Kutokuwepo kwa mahitaji kamilifu ya mradi;
v) Kufanyika kwa malipo yenye utata;
vi) Ripoti ya maendeleo haikujumuisha mambo yote muhimu kama vile usalama katika eneo la kazi, utunzaji wa mazingira na hatua stahiki, udhibiti wa vumbi, kelele na mambo na maambukizi ya virusi vya Ukimwi na ugonjwa na Ukimwi.




**(e) Ukamilishaji na ufungani wa miradi**

Kigezo hiki kilipima iwapo lengo lililokusudiwa lilifikiwa katika miradi.

Ukaguzi ulibaini upungufu kwenye miradi 35, uliochangiwa na ukosefu wa usanifu na michoro, kasoro kwenye maelezo ya kiufundi, usimamizi usioridhisha na matumizi ya vifaa visivyo sahihi.

Matokeo ya jumla yalionesha kuwa taasisi zilifikia kiwango cha kati kwa kupata wastani wa maksi 72.2. Hata hivyo, miradi 11 kati ya 186 iliyokaguliwa, ilipata alama mbaya.

Upungufu uliobainika katika ukamilishaji na ufungaji wa miradi ni kama ifuatavyo:

i) Kukosekana kwa ushahidi wa ukaguzi wa mwisho wa mradi au makabidhiano ya mradi;
ii) Kutoandaliwa kwa orodha maalum ya changamoto/vikwazo vilivyojitokeza wakati wa utekelezaji wa mradi.
iii) Kutoandaliwa kwa ripoti ya ukamilifu wa mradi.

## 3.6 Ukaguzi wa viashiria vya rushwa

### *3.6.1 Matokeo ya ukaguzi wa viashiria vya rushwa kwa taasisi 64 zilizokaguliwa*

Kati ya taasisi 70 zilizokaguliwa, taasisi sita zilibainika kuwa na viashiria vingi vya rushwa. Taasisi hizo ni Makumbusho ya Taifa, halmashauri ya Jiji la Dar es salaam, DART, TCRA, Ofisi ya Bunge na Wizara ya Maji na Umwagiliaji.




### *3.6.2 Matokeo ya tathmini ya viashiria vya rushwa kwa miradi*

Mamlaka ilifanya tathmini ya viashiria vya rushwa kwa kufanya ukaguzi wa thamani ya fedha kwenye miradi 20. Katika tathmini hiyo, miradi sita katika taasisi nunuzi tano ilibainika kuwa na uwezekano mkubwa wa viashiria vya rushwa. Taasisi zilizoonekana kuwa na uwezekano huo:

i) Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma;
ii) Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge;
iii) Makumbusho ya Taifa;
iv) Wizara ya Maji na Umwagiliaji; na
**v)** Wakala wa Nishati Vijijini (REA)

### *3.6.3 Malipo yenye utata*

Katika mwaka wa fedha 2015/16, ukaguzi ulibaini kuwa taasisi nne kati ya 157, zilifanya malipo ya shilingi 1.35 bilioni sawa na asilimia nne, kwa wakandarasi kwa kazi ambazo hazikufanywa. Taasisi hizo ni halmashauri ya jiji la Dar es Salaam, LAPF, REA na MOI.

### *3.6.4 Makusanyo ya ushuru wa halmashauri*

Mikataba 15 ya makusanyo ya ushuru ilikaguliwa kwenye halmashauri mbili. Ukaguzi huo ulibaini upungufu katika usimamizi wa miradi hiyo kwani kati ya shilingi 905.92 milioni zilizotarajiwa kukusanywa, ni shilingi 758.93 milioni, sawa na asilimia 83 ya matarajio, ndiyo pesa iliyowasilishwa kwenye halmashauri hizo. Aidha,

pamoja na ukweli kwamba makusanyo ya shilingi 146.99 milioni hayakuwasilishwa, halmashauri hizo hazikuchukua hatua yoyote juu ya jambo hilo.




### 3.7 Uhakiki wa malipo yenye utata kwa mwaka wa fedha 2014/15

Ukaguzi wa manunuzi uliofanywa na PPRA katika mwaka wa fedha 2014/15, ulibaini kuwa taasisi tisa zilifanya malipo yenye utata ya shilingi **951.71 milioni.** Taasisi hizo ni Tanapa, TRL, halmashauri ya jiji la Mwanza na halmashauri za wilaya za Kigoma, Kibondo, Misungwi, Tarime, Rungwe na Kyela.

Katika mwaka wa fedha 2015/16, PPRA ilifanya uhakiki wa malipo hayo yenye utata yanayokadiriwa kufikia shilingi 822.13 milioni kati ya shilingi 951.71 milioni zilizoripotiwa awali.

Hatahivyo, kati ya shilingi 822.13 milioni, ilibainika kuwa malipo ya shilingi 652.74 milioni hayakuwa ya utata kwa vile baadhi ya kazi zilikuwa kwenye utekekelezaji na kwa nyingine, zilikosekana nyaraka za kuhalalisha malipo, ambazo ziliwasilishwa wakati wa uhakiki huku baadhi ya malipo mengine yakifidiwa kutoka kwa malipo ya wakandarasi. Hivyo, jumla ya malipo yenye utata yalibaki kuwa shilingi 169.39 milioni.

# SURA YA NNE

## 4.0 CHANGAMOTO NA MATARAJIO

### 4.1 Changamoto

Kwa mwaka wa fedha 2015/16, kulikuwa na changamoto za kisekta na za ndani ya PPRA kama ifuatavyo:

#### 4.1.1 Changamoto za kisekta

a) Bei ya juu ya manunuzi ya vifaa, kazi za kandarasi na huduma kulinganisha na bei ya soko, gharama kubwa za mchakato wa manunuzi na mlolongo mrefu wa mchakato wa manunuzi, hivyo kusababisha matumizi mabaya ya fedha za umma, kuchelewa kukamilika kwa miradi na utoaji wa huduma kwa jamii;
b) Kukosekana kwa uadilifu na kiwango cha chini cha weledi miongoni mwa wafanyakazi wa umma na wazabuni na hivyo kuzuia upatikanaji wa thamani bora ya fedha;
c) Kukosekana kwa msawazisho wa bidhaa na huduma zinazotumiwa Serikalini;
d) Tofauti katika baadhi ya taratibu za manunuzi zinazotumiwa na halmashauri na zile za taasisi nyingine za Serikali, hivyo kuleta mgongano wa maslahi na ukiukwaji wa taratibu za manunuzi;
e) Kushindwa kuwasilisha ripoti kwa wakati na matumizi yasiyoridhisha ya mifumo ya PPRA, hivyo kuathiri ufuatiliaji wa shughuli za manunuzi ya taasisi husika;
f) Uhaba wa wafanyakazi katika taasisi zinazoshughulikia masuala ya manunuzi ya umma kuanzia ngazi ya usimamizi hadi utekelezaji;
g) Ufanisi mdogo kwa baadhi ya taasisi za umma katika kuendesha mchakato wa manunuzi na hivyo kusababisha ongezeko la gharama na muda katika utekelezaji wa miradi.
h) Baadhi ya watumishi wa umma na wazabuni kutokuwa na uelewa wa kutosha wa sheria ya manunuzi ya umma, hivyo kushindwa kufanya maamuzi sahihi katika michakato;
i) Baadhi ya taasisi kushindwa kuwasilisha taarifa za manunuzi yao PPRA kwa wakati, hivyo kuathiri mipango ya Serikali;
j) Upungufu wa kisheria katika kushughulikia masuala ya usalama pamoja na mengine na hivyo kucheleweesha utekelezaji wa mfumo wa manunuzi kwa njia ya mtandao; na
k) Baadhi ya taasisi za umma kutosimamia ipasavyo utekelezaji wa mikataba ya manunuzi, na hivyo kukwamisha upatikanaji wa thamani bora ya fedha.

#### 4.1.2 Changamoto za ndani ya PPRA

a) Uhaba wa rasilimali watu na fedha, hivyo kuathiri utekelezaji wa mpango mkakati wake;

b) Ukosefu wa jengo la ofisi na hivyo kusababisha gharama kubwa za uendeshaji kutokana na malipo ya kodi ya pango; na

**c)** Kushindwa kukidhi stahili za watumishi wake kwa wakati, hivyo kuathiri morali ya watumishi.

### 4.1.3 Mkakati wa kukabiliana na changamoto

Katika kukabiliana na changamoto zilizoainishwa, PPRA itachukua hatua zifuatazo:-

a) Kuendelea kutoa elimu kwa wadau kuhusiana na sheria ya manunuzi pamoja na mifumo na nyenzo za utekelezaji wa manunuzi;

b) Kushirikiana wadau wanaohusika na mfumo wa manunuzi kwa njia ya mtandao ili kuhakikisha kunakuwa na uelewa wa kutosha wa namna ya kuutumia mfumo huo;

c) Kufuatilia na kusimamia uzingatiaji wa sheria ya manunuzi na marekebisho yake;

d) Kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani na kuendelea kutangaza kazi zake ili kuongeza wigo wa mapato; na

e) Kuandaa wiki ya manunuzi ya umma pamoja na kufungua ofisi ya kanda katika jiji la Arusha kwa lengo la kuwafikia wadau kwa urahisi.